Powered By: www.manyamfranchise.com

## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Matokeo ya mtihani wa Kiswahili yamekuwa yakiyumba mwaka baada ya mwingine tangu kuanzishwa kwa mtaala mpya.Watahini wamekuwa wakishuhudia kushuka kwa viwango vya majibu yanayotolewa na watahiniwa .Kadhalika, kumekuwa na kushuka na kupanda kwa asilimia ya watahiniwa wanaotuzwa gredi za juu. Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika mtihani wa Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka minne (2009 hadi 2012 )

*Jedwali 9: Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (2009 – 2012)*

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganisho |
|---|---|---|---|---|---|
| 2009 | 1 | | 40 | 15.40 | 6.93 |
| | 2 | | 80 | 29.03 | 11.96 |
| | 3 | | 80 | 32.72 | 13.11 |
| | Jumla | 335,377 | 200 | 77.15 | 32.00 |
| 2010 | 1 | | 40 | 14.32 | 6.53 |
| | 2 | | 80 | 33.77 | 11.96 |
| | 3 | | 80 | 39.22 | 14.09 |
| | Jumla | 354,738 | 200 | 87.10 | 28.73 |
| 2011 | 1 | | 40 | 16.43 | 5.61 |
| | 2 | | 80 | 43.45 | 13.18 |
| | 3 | | 80 | 37.76 | 14.96 |
| | Jumla | 410,807 | 200 | 97.63 | 29.81 |
| 2012 | 1 | | 40 | 10.43 | 3.63 |
| | 2 | | 80 | 29.06 | 10.77 |
| | 3 | | 80 | 32.14 | 15.15 |
| | Jumla | 433,886 | 200 | 71.62 | 25.71 |

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

(i) Alama ya wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) ya mwaka wa 2012 imeshuka kutoka **16. 43** mwaka **2011** hadi **10.43** mwaka **2012.**

(ii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa katika karatasi hii ni **35/40.** Ni mtahiniwa **mmoja** tu aliyepata alama hii.

(iii) Idadi kubwa sana ya watahiniwa ilipata chini ya alama **20/40** katika karatasi ya kwanza.

(iv) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi katika karatasi ya kwanza ilikuwa **08/40.** Watahiniwa **81,121** , ndio waliotuzwa alama hii, huku watahiniwa **65,464** wakituzwa alama **07/40.** Hapa pana maana kwamba zaidi ya thuluthi ya watahiniwa wote ilipata baina ya alama **saba ( 07)** na **nane 08).**

(v) Karatasi ya kwanza haikuwaternga vyema wanafunzi bora na wale hafifu.Hili linadhihirishwa na alama tenganisho **(3.63)** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na alama ya tenganisho ya kikaida( **15.00).** Hali hii inaweza kusababishwa na watahini kuongozwa na kutawaliwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

(vi) Alama ya wastani ya karatasi ya pili ilishuka kutoka **43.45** mwaka **2011** hadi **29.06** mwaka **2012**.
(vii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **70/80.** Ni mwanafunzi **mmoja tu** aliyetuzwa alama hii.
(viii) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi katika karatasi hii ni **30/80.**Watahiniwa **15,559** ndio waliotuzwa alama hii.
(ix) Karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu.Alama tenganisho ilikuwa **10.77.**
(x) Matokeo ya karatasi ya pili (102/2) yamezidi kuyumba tangu mwaka wa **2009** .Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi(10)** mwaka **2010**, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka **2011**, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta thelathini (14.30** ) mwaka **2012**.
(xi) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2012 yameshuka kutoka **37.76** mwaka 2011 hadi **32.14** mwaka **2012** .
(xii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa katika karatasi hii ni **80/80.** Ni mtahiniwa **mmoja tu** aliyepata alama hii.
(xiii) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi ni **31/80.** Watahiniwa **10, 176** ndio waliotuzwa alama hii.

### 3.2.2 Uchanganuzi wa karatasi mahususi

### 3.2.3 Kiswahili Insha (102/1)

***Jedwali 10: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka ya 2009– 2012.***

| Mwaka | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 15.40 | 14.32 | 16.43 | 10.43 |
| Alama ya Tenganisho | 6.93 | 6.53 | 5.61 | 3.63 |

Jedwali hili laonyesha kwamba katika kipindi cha miaka hii minne, (2009-2012), matokeo ya karatasi ya 102/1 yamekuwa yakiyumba , na kwamba watahiniwa wengi hawajaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 40. Katika mwaka wa 2012, matokeo yalishuka kwa alama **6.00.**

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

**1 Lazima**:

Wewe ni mkuu wa Baraza la Wanafunzi shuleni mwenu. Kumekuwa na visa vya wanafunzi kukiuka sheria za shule. Andika kumbukumbu za mkutano wa baraza hili uliofanyika kujadili suala hili.

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika kumbukumbu za mkutano wa Baraza la Wanafunzi kuhusu ukiukaji wa sheria za shule. Asilimia kubwa ya watahiniwa ilizingatia muundo wa juu wa kukumbukumbu.Hata hivyo idadi kubwa ya watahiniwa haikumudu muundo wa ndani wa kumbukumbu. Wengi mno walishindwa kuyajadili masuala jinsi yanavyojadiliwa katika vikao halisi vya mikutano ya aina hii. Baadhi waliandika kana kwamba wanaandika ripoti.Isitoshe, watahiniwa wengi walishindwa kudondoa na kujadili hoja.Walieleza tu kijumla na kujikosesha alama.

Tungo za watahiniwa zilidhihirisha kwamba wengi wamekosa ubunifu.Hata katika sehemu ya yanayotokana na kumbukumbu za mkutano uliotangulia wengi waliandika mambo yasiyohusiana na mada badala ya kujikita kwenye mada waliyopewa. Kadhalika, watahiniwa wengi hawakuzingatia idadi ya maneno waliyoagizwa kutumia.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine, hususan swali la nne ambalo ndilo lililojibiwa na wengi.

**Ushauri kwa walimu**

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi, kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Elimu.

**Mapendekezo**

(i) Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.
(ii) Walimu watumie silabasi za K.I.E na K.N.E.C katika ufundishaji wao.
(iii) Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa mapana (magazeti, majarida na vitabu katika nyanja anuwai) ili kujifahamisha kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa. Hili litakuza ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala nyeti/masuala ibuka iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.
(iv) Wanafunzi wahamasishwe kufasiri maswali kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.

### 3.2.4 Kiswahili Lugha (102/2)

***Jedwali 11: Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka ya 2009 hadi 2012.***

| **Mwaka** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** |
|---|---|---|---|---|
| **Alama ya Wastani** | 29.03 | 33.77 | 43.45 | 29.06 |
| **Alama ya Tenganisho** | 11.96 | 14.09 | 13.18 | 10.77 |

(i) Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameshuka mwaka wa 2012 kwa alama **14.39.**

(ii) Maswali nambari **tatu** na **nne** ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa wengi zaidi.

Chunguza uchanganuzi wa maswali haya.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

**Swali la 3:**

**3 MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

(a) Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno. (alama 2)

(b) Onyesha matumizi ya kiambishi **'ku'** katika sentensi ifuatayo:
Amani atakutengenezea mpini wa jembe kisha aelekee kule kwao. (alama 2)

(c) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo: (alama 2)
(i) Irabu ya mbele, wastani .....
(ii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini .....

(d) Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya YA - YA kutunga sentensi. (alama 2)

(e) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali timilifu. (alama 2)

(f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)
KN (N) + KT (T + E) + U + KN (N) + KT (T + E)

(g) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi changamano. (alama 2)

(h) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: **koga** na **konga**. (alama 2)

(i) Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na nomino ya jamii. (alama 2)

(j) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (alama 3)

(i) nywa (tendesha) .....

(ii) la (tendeana).....

(iii) vaa (tendwa) .....

(k) Akifisha sentensi ifuatayo kubainisha dhana **tatu** tofauti.
Julius Kiptoo mwanawe Kung'u na Justine walikiletea kijiji chao sifa. (alama 3)

(l) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.
Naam, ameleta machache. (alama 2)

(m) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu. (alama 2)

(n) (i) Eleza maana ya shadda. (alama 1)

(ii) Onyesha panapotokea shadda katika neno: ' mteremko'. (alama 1)

(o) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Sahibu yake alishikwa na kisunzi.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

(p) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari.
Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye misimano thabiti mno.
(alama 3)

(q) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.
" Shughuli yetu itamalizika kesho, " mama alimwambia Juma. (alama 2)

(r) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo:
Watahiniwa hao walisoma maswali yote kwa makini. (alama 2)

(s) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu/dhamira yake.

Funga majani matano matano kwa kila fungu. (alama 1)

Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa na silabasi. Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi kujibu maswali aliyopewa. Watahiniwa wengi sana walishindwa kumudu dhana za kimsingi za kisarufi kama vile uandishi katika usemi wa taarifa.Kadhalika ilibainika kwamba watahiniwa wengi hawaelewi istilahi maalum za kuulizia maswali.Kwa mfano neno **'ainisha'** lilichukuliwa na wengi kuwa **'changanua'.**

**Majibu**

3. (a)
- Mzizi wa neno ni sehemu ya neno inayobeba maana ya kimsingi/maana ya kileksia ya neno.
- Sehemu hii haibadiliki hata neno likinyambuliwa / likiambishwa.
mfano: soma, gand-a, sahau-liw-a, ag - a kimbi-li-a, baba, kuku, tak - a
Sehemu zilizopigiwa mstari ndizo mizizi ya maneno husika.

Kueleza - 1, mfano 1 = alama 2

**Tanbihi**

Kuna mizizi huru (kama vile baba, mama, zuri, sahau) na mizizi tegemezi/funge (kama vile som katika soma). Mtahiniwa anaweza kutoa mfano wowote, mradi asadikishe anaelewa dhana ya mzizi.

(b)
- Ata**ku**tengenezea - nafsi ya pili (umoja) / mtendewa /yambwa tendewa (kitondo).
- **ku**le - mahali kusikodhihirika/kiambishi cha ngeli ya mahali. (Ku - Ku) (Kitundu)

(alama 1)

(c) (i) Irabu ya mbele, wastani. /e/ (alama 1)
(ii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini. /g/ (alama 1)

(d) Marashi yaya haya / haya haya ndiyo aliyonunuliwa. (alama 2)
Nomino nyingine: mate, maziwa, mafuta, mazingira n.k.

(e) Maisha ya**li**kuwa ya**me**mwendea vyema. (viambishi li, me) (alama 2)

(f) **Mifano**:
- Mandu huandika vyema lakini Kani huandika vibaya.
- Maskauti walitembea kijeshi ila wanafunzi hawakuvutiwa kamwe.
- Maria atasafiri kesho ilhali Zaina atasafiri mtondo.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Mwalimu alituita tena lakini Komu hakuitika katu.
- Terry alielekea kushoto na Ndua alibaki katikati.

**Tanbihi** (alama 2 / 0)

(i) Hii ni sentensi ambatano.
(ii) Mtahiniwa **lazima** abainishe muundo wa sentensi ambatano.
(iii) Mtahiniwa akikosa sehemu moja atuzwe sufuri (0).
(iv) Aina yoyote ya kielezi inaweza kutumiwa mradi mtahiniwa abainishe mpangilio ufaao wa maneno.
(v) Viunganishi ambatani vitumiwe/asitumie viunganishi vitegemezi.

(g) - Sentensi changamano huwa na kishazi kimoja huru na kingine kitegemezi.
- Huweza kuwa na vishazi vyote viwili vitegemezi.
- Vishazi huunganishwa kwa viunganishi vitegemezi kama vile, ikiwa, kama, ingawa, iwapo, ki, nge, ngali, ka virejeshi k.v. amba na 'o' rejeshi, n.k.

**Mifano**
- Jamvi lililonunuliwa limechakaa.
- Usahihishaji ukimalizika mapema wanafunzi watapata matokeo.
- Wafanyakazi walijitahidi wakamaliza kazi mapema.
- Ingawa alikuwa maskini aliwaelimisha watoto wake wote.
- Mvua ingalinyesha mapema tungalipata mavuno bora.
- Kama unataka kumwona daktari njoo mapema.

(h) Koga
- uchafu
- fanya maringo
- ondoa uchafu mwilini kwa kutumia maji na sabuni

Konga
- kuzeeka
- kunywa kinywaji/ maji ili **kupunguza kiu**
- kusanya pamoja/ kukutanisha watu pamoja

**Tanbihi**
Mtahiniwa anaweza kutumia / kuibua maana yoyote mradi kila mojawapo ibainike katika sentensi.

(i) Nomino dhahania - utu, furaha, urembo, wepesi, wema, wivu.

1 x 1 = alama 1

Nomino ya jamii - Kikosi, mkungu, chane, funda, tano, darasa, mfano - darasa la wanafunzi, jeshi, kikosi, umati, halaiki, timu, jamii, familia, hadhira n.k.

1 x 1 = alama 1

(j) (i) Nywa - nywesha/nywisha
(ii) La - liana
(iii) Vaa - valiwa

(k) **Mifano**
- Julius Kiptoo, mwanawe Kung'u na Justine walikiletea kijiji chao sifa. (Wahusika

Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

watatu)

- Julius Kiptoo (mwanawe Kung'u) na Justina walikiletea kijiji chao sifa. (Wahusika wawili) (Julius Kiptoo ni mwana wa Kung'u)
- Julius Kiptoo, mwanawe, Kung'u na Justina walikileta kijiji chao sifa. (Wahusika wanne). (mwanawe - mwana wa Julius Kiptoo au mtu mwingine)
- Julius, Kiptoo (mwanawe Kung'u na Justina)walikiletea kijiji chao sifa. (Wahusika wawili). (Kiptoo ni mwana wa Kung'u na Justina)

**Tanbihi**

(i) Huu ni mfano wa sentensi tata.
(ii) Lazima dhana tatu zijitokeze.
(iii) Mtahiniwa si lazima / hahitajiki kuelezea maana, viakifishi vinatosha.

(l) Naam- kihisishi

Machache - kiwakilishi / kiwakilishi cha idadi ya jumla. (alama 1)

(m)
- Muli alikuwa mwalimu wetu.
- Huyu anaonekana mzima.
- Teddy amekuwa mpole.
- Swali limetuwia gumu.

(alama 2)

(Kitenzi kiwe na kiambishi nafsi au cha ngeli na cha wakati au cha hali)

(n) (i) Shadda ni mkazo unaotiwa katika neno au silabi wakati wa kutamka (alama 1)

(ii) m-te-re-'m-ko (alama 1)

**Tanbihi**

- Mkazo utiwe kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa neno.
- Si lazima atenge silabi.
- Anaweza kupigia mstari

(o) Sahibu - rafiki /mwandani (alama 1)
Kisunzi - kizunguzungu/ kisulisuli (alama 1)

(p) - wa kijinsia - kirai (ki) husishi (neno kuu ni kihusishi 'wa') (alama 1)

- viongozi wenye msimamo (kirai nomino) (neno kuu ni nomino: viongozi) (alama 1)

- thabiti mno - kirai(ki) vumishi
(neno kuu ni kivumishii 'thabiti'
(alama 1)

**Tanbihi**

- Uainishaji ufanywe **kimuundo** wala si **kimajukumu**. Kwa mfano, 'wa kijinsia' ni kirai husishi wala **si** kirai vumishi, japo kinafanya kazi kama kivumishi.

(q) Mama alimwambia Juma kwamba shughuli yao ingemalizika siku ambayo ingefuata. (alama 2/0)

(r) - kiima - watahiniwa hao (alama 1)



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

- chagizo - kwa makini (alama 1)

**Tanbihi**

- **Kiima** ni sehemu ya sentensi ambayo ndiyo habari zake zinatolewa katika kiarifu cha sentensi. Aghalabu huwa kikundi nomino ambacho hutokea kabla ya kitenzi, na kwa kawaida huwa ndicho mtenda katika sentensi.

**Chagizo** ni sehemu ya sentensi ambayo huja baada ya kitenzi au yambwa. Huwa kielezi/ kirai elezi au hata kirai husishi ambacho kinafanya kazi kama kielezi. Ni sehemu ya ziada katika sentensi na huweza kuondolewa bila kuathiri maana ya kimsingi ya sentensi.

(s) Sentensi agizi / amrishi / amri

(inatoa maagizo / maelekezo)

1 x 1 = 1

**Swali la nne:**

**4. ISIMUJAMII** (Alama 10)

Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha.

(a) Mazingira (alama 4)

(b) Madhumuni (alama 2)

(c) Malezi (alama 4)

Swali hili lilikuwa na sehemu tatu ambazo zilimhitaji mtahiniwa kujadili jinsi vipengele vya kijamii kama vile mazingira, malezi na madhumuni vinavyoathiri mitindo ya lugha.Watahiniwa wengi mno walishindwa kutumia ujuzi wao wa kaida zinazotawala matumizi ya lugha katika jamii kujibia swali hili.

Imebainika kuwa watahiniwa wengi hawayamudu maswali yanayowahitaji kutumia stadi ya utekelezaji/matumizi. Aidha, uchunguzi umeonyesha kwamba mada na dhana ya Isimujamii na mawanda yanayostahili kuzingatiwa katika shule za upili bado yanawatatiza walimu na wanafunzi. Kadhalika, imebainika kuwa asilimia kubwa ya walimu haitumii silabasi, hivyo haidiriki kujua mada na dhana zinazopaswa kufundishwa katika kiwango hiki.Walimu wengi mno hutegemea vitabu vya kiada vilivyopendekezwa na Wizara ya Elimu ambavyo huenda vikakosa kushughulikia baadhi ya mada.

**Majibu**

4. Mazingira

- Mzungumzaji huchota msamiati kutoka mahali anapozungumzia. Kwa mfano, atatumia msamiati wa sokoni akiwa sokoni. Pia kuna lugha ya mahakamani, kwenye mazishi, maabadini n.k.
- Mazingira huathiri kiimbo na hata kidatu. Kwa mfano, mtu akiwa darasani huzungumza kwa kidatu cha chini.

- Mazingira huathiri uteuzi wa msimbo/lugha/lahaja ambayo mtu anatumia. Kwa mfano, mazingira rasmi humtaka mtu kutumia lugha rasmi kama vile Kiingereza na Kiswahili sanifu.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Mazingira hudhibiti kiwango cha usanifu na urasmi wa lugha. Kwa mfano, mazingira yasiyo rasmi hayahitaji kutumia lugha yenye urasmi au usanifu, mtu anaweza kutumia hata simo/ misimu.

- Mazingira hudhibiti mtindo nafsi wa mtu. Kwa mfano, mtu katika mnada au biashara ya rejareja huweza kujirudiarudia ili kuwavutia wateja.

- Ishara anazotumia mtu hudhibitiwa na mazingira. Zipo ishara nyingine za uso au hata miondoko ambayo haikubaliwi/ni mwiko katika baadhi ya tamaduni / mazingira.

- Mtu anayeishi katika mazingira magumu / makali / ya unyanyasaji huelekea kutumia lugha kali au pengine ya matusi, pengine ili kujihami.

4 x 1 = 4

(b) Madhumuni

- Lengo la mawasiliano huathiri jinsi mtu anavyotumia lugha. Kwa mfano, mtu anapoonya hutumia lugha yenye toni kali. Anapotaka kushawishi hutumia lugha ya upole.

- Madhumuni huathiri uteuzi wa msimbo/lahaja/lugha, Kwa mfano, kiongozi anapotaka kuonyesha utangamano na mwanakijiji mwenzake huelekea kutumia lugha ya mama badala ya Kiingereza au hata Kiswahili. Kiongozi huyo huyo huelekea kutumia Kiingereza anapotaka kumtenga mwanakijiji mwenzake.

- Madhumuni huathiri kiimbo na shadda. Mtu anapotaka kusisitiza jambo hutia shadda kwenye maneno, au dhana anazotaka kusisitiza. Wakati mwingine hupandisha sauti ili kuwiana na hali ya msisitizo.

2 x 1 = 2

(c) Malezi

- Mtoto aliyelelewa kwa kudhibitiwa huinukia kutoweza/kutomudu kujieleza vyema kwa sababu ya woga aliojazwa.
- Mtoto aliyelelewa katika mazingira ya unyanyasaji hutumia lugha kali ya kujihami.
- Mtoto akilelewa na wazazi wnaozungumza lugha mbili/zaidi ya mbili huweza kujifunza/ kutumia lugha zote mbili.
- Mtoto aliyelelewa akihimizwa kujieleza huinukia kuwa na uwezo/ukakamavu wa kujieleza.
- Mtoto asipofunzwa lugha ya mama hushindwa kujieleza kwa lugha hiyo.
- Mtoto hufunzwa kuepuka matumizi ya msamiati/lugha ya aibu/kali, kwa hivyo kutoitumia katika mazungumzo.

4 x 1

**Tanbihi**
Sheria na kaida zote za usahihishaji wa karatasi hii zitumike.

Ni muhimu kutaja kuwa baadhi ya watahiniwa pia walikuwa na changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu, hasa yale ya kiutekelezaji. Isitoshe, wapo walioshindwa kuyasanisi mawazo kuunda tungo zilizohitajika katika jaribio la ufupisho.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

**MAPENDEKEZO**

(i) Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi katika vipengele vyote vya kisarufi.
(ii) Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi/ utekelezaji na usanisi .Wasitarajie kila mara kupata maswali ya kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye vifungu au kukariri kutoka kumbukumbu zao.
(iii) Wanafunzi wapewe mazoezi ya ufahamu na muhtasari mara kwa mara huku mtiririko ufaao ukisisitizwa ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.
(iv) Walimu wasisitize vipengele vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.
(v) Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe zaidi. Mathalan mwalimu anaweza kutumia fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi.Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.
(vi) Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.
(vii) Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wake bila kubagua.

### 3.2.5 Kiswahili Fasihi (102/3)

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2009 hadi 2012.

| **Mwaka** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 32.72 | 39.22 | 37.76 | 32.14 |
| Alama ya Tanganisho | 13.11 | 14.09 | 14.96 | 15.15 |

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3 mwaka wa 2012 yameshuka kutoka alama ya wastani **37.76** mwaka wa 2011 hadi **32.14** mwaka wa 2012.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.

**Swali la kwanza**

**1** (a) Eleza nafsi ya usimulizi iliyotumiwa katika hadithi ya "Mkimbizi". (alama 3)

(b) Bainisha mifano **mitatu** ya mbinu rejeshi katika hadithi hii na ueleze umuhimu wa kila mojawapo. (alama 9)

(c) "Ukimbizi ni kikwazo cha maendeleo." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi hii. (alama 8)

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa :
a) Kutumia ujuzi wake wa vipengel;e vya uchanganuzi wa kazi za kinathari, hususan kipengele cha kimuundo ambacho kilitahini nafsi ya usimulizi na mbinu rejeshi.
b) Kutumia ujuzi wake wa yaliyomo katika hadithi ya 'Mkimbizi' kuonyesha athari za ukimbizi.

Hata hivyo, ilidhihirika kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haielewi maana ya mbinu rejeshi, hivyo haikumudu kujibu swali ipasavyo. Kadhalika watahiniwa wengi mno walijadili athari za ukimbizi kwa jumla bila kuzingatia hadithi husika.Haya huenda yalisababishwa na hali ya watahiniwa kutokuwa



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

na makini ya kusoma swali na kubaini kiini hasa cha swali. Pia ilibainika kwamba watahiniwa wengi bado wana mtazamo hasi kuhusu ushairi .Ni watahiniwa wachache tu waliofanya maswali ya ushairi. Watahiniwa hawa hawakupata alama za juu.

**Majibu**

1. (a) - Hadithi hii inasimuliwa katika nafsi ya kwanza. Usimulizi huu unafanywa na mhusika mtoto/kijana.
- Msimulizi ni mhusika mmojawapo wa hadithini.
- Kuna matumizi ya mofu (ni) na (tu) za nafsi ya kwanza.

kutaja - alama 1
maelezo - alama 2
Jumla - alama 3

(b) Mifano mitatu ya mbinu rejeshi na umuhimu wayo.

(i) Maelezo ya Msimulizi kuhusu usiku ambao babake na watu wengine walizungumza kuhusu mzozo baina ya Wahutu na Watutsi. Babake aliuma kidole. Aidha tunaelezwa kuwa Msimulizi ambaye ni Mhutu alicheza na watoto wengine waliokuwa Watutsi bila kuona tofauti.
Hapa mbinu rejeshi inaonyesha kuwa:
- Watoto hawakuhusika na tofauti za kikabila.
- Watu wazima ndio wenye kuhusika na tofauti za kikabila.
- Mzozo baina ya Wahutu na Watutsi ni jambo lililopangiwa kikamilifu.
- Vita huwatia wasiwasi hata watu wazima.
- Pia mbinu rejeshi inaibua maudhui ya ubaguzi, na uzalendo.

kutaja - alama 1
umuhimu 2 x 1 = 2
Jumla - alama 3

(ii) Msimulizi anakumbuka kuhusu maisha yao shuleni ambapo alisoma na Jesse: UK 119

Umuhimu wake:
- Kuonyesha kuwa msimulizi na Jesse walikuwa na uhusiano mzuri.
- Wote walikuwa hodari katika masomo ya lugha (Kinyarwanda (Jesse) Kifaransa (Msimulizi) (maudhui ya bidii)
- Athari ya ukimbizi - wanaachishwa masomo.

kutaja - alama 1
umuhimu - 1 x 2= 2
Jumla - alama 3

(iii) Msimulizi anawaza kuhusu wema wa Jesse baada ya Jesse kufa. UK 122
Anakumbuka uhusiano wao mwema wakiwa shuleni Rugifare.

Umuhimu wake:
- inaonyesha uhusiano wa kidugu baina yao.
- imani ya Jesse - anamletea musimulizi njugu shuleni.
- kuonyesha mshikamano wa kijamii - wanacheza pamoja.
- kuonyesha dhiki ya kisaikolojia inayosababishwa na ukimbizi.

kutaja - alama 1
umuhimu - 1 x 2= 2
Jumla - alama 3



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

(iv) Msimulizi akiwa safarini kuelekea ng'ambo anakumbuka maneno ya Savalanga, anakumbuka kilio cha uchungu cha mamake na hali iliyomfanya kuwa mkimbizi. (UK 124)

(v) Msimulizi anakumbuka sura ya mama na ndugu zakeakiwa Befinga (UK 122).

Umuhimu wake:
- Kuonyesha dhiki ya kisakolojia inayochechewa na vita.
- Kuonyesha maafa yanayosababishwa na vita.

Umuhimu
- inaonyesha uzalendo wa Msimulizi. Anakumbuka kwao, anawazia wasia wa Savalanga.
- inafumbata maudhui ya ujenzi wa jamii mpya kwa kutarajia kutimiza aliyoambiwa na Savalanga.

kutaja - alama 1
umuhimu - alama2
Jumla - alama 3

**Tanbihi**

(i) Mtahiniwa aonyeshe alipo sasa na kusimulia tuku la nyuma.
(ii) Mtahiniwa afafanue kikamilifu mifano yoyote mitatu ili kutuzwa alama 9.

(c) Vikwazo vinavyoletwa na ukimbizi.

- Kukatizwa kwa elimu - Jesse na Msimulizi wanaacha masomo yao na kukimbilia usalama. (Athari katika sekta ya elimu).
- Kusambaratika kwa familia. Baba ya Msimulizi anaenda vitani.
- Utegemezi. Wakimbizi wanategemea hifadhi/makao katika nchi nyingine. Wakimbizi wanapiga kambi mpakani/kuwa mzigo kwa majirani.
- Ukosefu wa usalama wa chakula. Wanakula matunda-mwitu na wanyama-mwitu, hata mizoga! Uhamishoni chakula ni haba, wanang'angania chakula.
- Wasiwasi/ ukosefu wa utulivu/ ukosefu wa amani. Kila mara wanahofia kushambuliwa. Hofu inamfanya Msimulizi kujikojolea.
- Vifo vya watu ambao wanachangia maendeleo ya nchi- Jesse/ Savalanga, wakimbizi waliouawa njiani.
- Magonjwa hali duni ya afya, pale kambini/njiani. Jesse na Savalanga wanakufa kwa ugonjwa.
- Dhiki/athari za kisaikolojia. Msimulizi anasikia milio ya bunduki akilini.
- Kutegemea kuelimishwa na jamii nyingine. Msimulizi na wenzake tisa wanapelekwa ng'ambo kusoma.
- Ukosefu wa mshikamano wa kijamii - njiani wanapoulizwa kama wao ni Wahutu au Watutsi wanajawa na woga.
- Hisia za ukiwa - msimulizi anasema walimhurumia Savalanga kwa kupoteza aila yake, hali ambayo inaathiri utulivu wa mtu binafsi.
- Nchi inaachwa bila raia wenye nguvu kuijenga upya. Mzee Savalanga anaonekana kukata tamaa, ndio maana anamuusia msimulizi kurudi nyumbani baada ya vita ili



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

kujenga jamii upya.
- Ukimbizi unaathiri uongozi. Nchi inapoteza vijana kama vile Jesse ambao wangechangia kubaðilisha hali ya siasa nchini kwa vile hao hawakutawaliwa na mawazo ya ukabila.
- Makazi duni - njiani na kambini.

(4 x 2 = alama 8)

### 3.2.6 MAPENDEKEZO

3.2.6.1 Walimu wafundishe vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu wake huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:
(i) Dhamira na maudhui
(ii) Fani, kama vile:
- Mandhari
- Ploti
- Usimulizi
- Wahusika
- Muundo
- Mtindo, kama vile tamathali za usemi, urudiaji, n.k

3.2.6.2 Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika diwani teule ya hadithi fupi.

3.2.6.3 Wanafunzi wawekewe misingi bora katika fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza.

3.2.6.4 Walimu wawafundishe wanafunzi wao istilahi muhimu zinazohusiana na ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya ushairi.

### 3.2.7. Uchanganuzi wa mtihani wa Kiswahili kwa jumla

Uchanganuzi wa mtihani wa mwaka wa 2012 umebainisha kwamba:

3.2.7.1 Alama ya wastani ya somo la Kiswahili imeshuka kutoka **97.63** mwaka 2011 hadi **71.62** mwaka **2012** . Hii ndiyo alama ya wastani ya chini zaidi tangu mwaka wa 2009.
3.2.7.2 Alama wastani ya somo hili imekuwa ikiyumba tangu mwaka wa 2009.
3.2.7.3 Alama ya juu iliyotuzwa katika somo hili ni **165/200.**Ni mwanafunzi **mmoja** tu aliyepata alama hii.
3.2.7.4 Ni asilimia ndogo sana ya watahiniwa iliyopata gredi wastani **A** na **A-** katika somo hili.

### Hitimisho

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba matokeo ya somo la Kiswahili yanazidi kushuka. Ni watahiniwa wachache mno waliofikia viwango vya juu vya utendaji katika karatasi zote tatu.

Ni matumaini yetu kwamba walimu na wanafunzi watafaidi kwa uchanganuzi uliotolewa .Kadhalika tunawahimiza kuyatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuimarisha matokeo ya somo hili.



Powered By: www.manyamfranchise.com